

# CHANJO YA COVID-19 MASWALI NA MAJIBU

Ili kukomesha janga hili, tunahitaji kutumia vifaa vyetu vyote vya uzuiaji. Chanjo ni mojawapo ya vifaa bora zaidi vya kuinga afya yako na kuzuia ugonjwa. Tafiti zinaonyesha kuwa chanjo za COVID-19 zinafanya kazi vizuri zaidi kukuzuia kupata COVID-19. Kuchanjwa kikamilifu dhidi ya COVID-19 kunaweza kusaidia kukuzuia kuugua vibaya zaidi ukipata COVID-19.

Je, tulitengeneza vipi chanjo ya COVID-19 haraka hivyo?



Je, ni vipi ilivyoidhinishwa haraka kuliko chanjo nyingine?

Je, chanjo inaweza kusababisha COVID-19, kubadilisha DNA yangu, kusababisha utasa au ugumba au kuweka maikrochipu?



Ikiwa tayari nilikuwa na COVID-19 na kupona, ninahitaji chanjo?



Kwa nini ninapaswa kupata chanjo ya COVID-19?



Je, chanjo ya COVID-19 husababisha madhara baada ya chanjo?



Chanjo ya COVID-19 ni salama na faafu. Maarifa yanayotumiwa kuzitengeneza yanatokana na utafiti na sayansi ya zaidi ya miongo 2. Chanjo hizi husaidia mfumo wetu wa kingamaradhi kupambana na virusi vinavyosababisha COVID-19 endapo tutaambukizwa siku zijazo. Hivi ndivyo chanjo nyingi zinavyofanya kazi!

Mchakato wa Emergency Use Authorization (Idhini ya Matumizi ya Dharura, EUA) nchini Marekani ni wa kina sana. Mapitio mapana yanafanywa ili kuhakikisha kuwa chanjo zinatimiza viwango vya usalama na ufaafu.

Chanzo: [cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/distributing/steps-ensure-safety.html](https://cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/distributing/steps-ensure-safety.html)

Chanjo zinazotumika Marekani (na nyingine zote duniani) hazina virusi hai vinavyosababisha COVID-19. Haziwezi kukupa COVID-19, kubadilisha DNA yako wala kusababisha utasa wala ugumba. Chanjo HAZINA maikrochipu wala vifaa vya ufuatiliaji.

NDIYO, bado unapaswa kupata chanjo ya COVID-19. Chanjo inaimarisha mkabiliano wako wa kingamaradhi ili kukuinga vizuri zaidi.

Kwa maelezo zaidi tembelea:

[cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/vaccine-benefits.html](https://cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/vaccine-benefits.html)

Chanjo ni salama, faafu (85-95% kulingana na aina), BILA MALIPO na ni njia bora ya kurejesha kiwango cha kawaida katika maisha yetu, husaidia kufufua uchumi wetu na kuokoa maisha.

Madhara baada ya chanjo ni ishara za kawaida kuwa mwili wako unajenga kinga. Madhara haya ya baada ya chanjo kwa kawaida hutoweka baada ya saa 24-48. Madhara maarufu zaidi baada ya chanjo ni maumivu ya misuli, homa ya baridi, homa, maumivu ya kichwa, kichefuchefu, uchovu, maumivu na uvimbe kwenye sehemu ya mkono uliyodungwa sindano. Watu wengine hushuhudia mikabiliano hii. Ikiwa huna madhara baada ya chanjo, haimaanishi kuwa mwili wako haujengi kingamaradhi. Kila mtu huwa na mkabiliano tofauti. Wasiliana na daktari wako ili kuripoti na kujadili madhara yako baada ya chanjo ikiwa una wasiwasi.

Kwa maelezo zaidi tembelea:

[cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/expect/after.html](https://cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/expect/after.html)



Kliniki ya Kaunti ya Onondaga inayotoa Chanjo ya COVID-19: 315.435.2000  
au pata chanjo karibu nawe kwenye [vaccines.gov/search](https://vaccines.gov/search)

Kuchanjwa na kufuata mapendekezo ya CDC ili kujikinga mwenyewe na wengine kutatoa kinga bora dhidi ya COVID-19.



**ongovhealth**  
**Onondaga County**  
**Health Department**

[ongov.net/health](https://ongov.net/health) · [facebook.com/ongovhealth](https://facebook.com/ongovhealth)